THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
Kenya Certificate of Secondary Education

# 102/3 – KISWAHILI – Karatasi ya 3

## FASIHI

## Nov. 2018 – Muda: Saa 2½

Jina .................................................. Nambari ya Mtahiniwa ......................................

Sahihi ............................................... Tarehe ..............................................................

**Maagizo**

(a) *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
(b) *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
(c) *Jibu maswali* ***manne*** *pekee.*
(d) *Swali la* ***kwanza*** *ni la* ***lazima.***
(e) *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani: Riwaya, Tamthilia, Hadithi Fupi na Fasihi Simulizi.*
(f) *Usijibu maswali* ***mawili*** *kutoka* ***sehemu moja.***
(g) *Majibu yote* ***lazima*** *yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
(h) *Majibu yote* ***sharti*** *yaandikwe kwenye nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
(i) ***Karatasi hii ina kurasa 24 zilizopigwa chapa.***
(j) ***Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.***

**Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | Jumla | |

© 2018 The Kenya National Examinations Council


918294

Geuza ukurasa

## SEHEMU A : USHAIRI

1. **Lazima**

A. Mazrui: *Chembe Cha Moyo*
*Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

Nimeyaandika maneno haya
    Kwa niaba ya:
    Mamilioni wasio malazi
    wabebao vifurushi vilivyo wazi
    wazungukao barabarani bila mavazi
    ...milki yao ya maisha.
Kwa niaba ya:
Maelfu wanouawa bila haki
wiki baada ya wiki
    leo sumu au spaki
    leo kamba au bunduki
na kwa wale wanosubiri kunyongwa.

Kwa niaba ya:
Vijana walio mitaani
wale mayatima wa maskini
wazungukao mapipani
kila pembe mjini
kuokota sumu kutia tumboni
kujiua bila kujua
ili kupata kuishi.

Kwa niaba ya:
Wakongwe wasiojiweza
walao chakula kilichooza
wachukuao choo wakijipakaza
polepole wakijiangamiza
katika vyumba vyao
baridi na giza
kwa sababu hawana watazama
wala wauguza.

Kwa niaba ya:
Waishi na nyingi hofu
kwa sababu ya madawa tifutifu
yatiwayo vyakulani yakitufanya wafu
bila ya mtu kuona
    kama kwanba sote tu vipofu,

Na kwa niaba yetu sote;
Tuliofungwa vifungoni, duniani
Tuliosukumwa kingoni, maishani
Tuliopokonywa maoni, machoni
Tuliotiliwa sumu, malishoni
Tuliodidimizwa kinyesini
ili 'maendeleo'
yaendelee kwenda njiani
huku yakitema machicha ya roho zetu.

(a) "Shairi hili linakatisha tamaa." Thibitisha kauli hii kwa kutoa mifano **saba** kutoka kwenye shairi. ( alama 7)

(b) Fafanua umuhimu wa aina **mbili** za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 4)

(c) Bainisha vipengele vifuatavyo vya kimtindo katika shairi hili. (alama 3)

(i) tasfida

(ii) kinaya

(iii) tashihisi

(d) Eleza kwa kutoa mfano, mbinu **moja** ambayo mshairi ametumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi katika ubeti wa **tano.** (alama 2)

(e) Andika ubeti wa **pili** kwa lugha ya nathari. (alama 2)

(f) Bainisha nafsineni katika shairi hili. (alama 2)

## SEHEMU B: RIWAYA

**K. Walibora:** *Kidagaa Kimemwozea*

*Jibu swali la 2 au la 3.*

**2.** "Riwaya hii ya aina yake inathibitisha kwa usanii wa kupigiwa mfano jinsi ndoto ya uhuru barani Afrika imegeuka kuwa jinamizi."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Onyesha jinsi ndoto ya uhuru barani Afrika imegeuka kuwa jinamizi kwa kuwarejelea wahusika wafuatao:

(i) Majisifu (alama 8)

(ii) Fao (alama 4)

(iii) Wahudumu katika zahanati ya Nasaba Bora (alama 4)

3. (a) "Leo usukani uko mikononi mwetu wenyewe. Mbeberu amekwisha ng'olewa pamoja na mizizi yake."

Onyesha kinaya katika kauli hii kwa kutoa mifano **kumi** kutoka *Kidagaa Kimemwozea.* (alama 10)

(b) Tathmini mchango wa wanyonge katika kuzoroteka kwa hali ya maisha yao. (alama 10)

## SEHEMU C: TAMTHILIA

**P. Kea:** *Kigogo*

*Jibu swali la 4 au la 5.*

4. Tusiwaruhusu watu wachache waliojazwa kasumba za kikoloni kuturejesha kwenye utumwa. Hatuwezi kukubali kutawaliwa kidhalimu tena!"

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Fafanua kinyume kinachojitokeza katika kauli iliyopigiwa mstari kwa kurejelea hoja **kumi na sita** kutoka kwenye tamthilia hii. ( alama 16)

5. "Si haki! Unayazika matumaini yetu. Unaifukia kesho yetu."

(a) Fafanua umuhimu wa mzungumzaji wa maneno haya katika kuijenga tamthilia ya *Kigogo.* (alama 6)

(b) Kwa kurejelea hoja **kumi na nne** kutoka kwenye tamthilia, jadili namna uongozi wa Sagamoyo unavyoyazika matumaini ya raia. (alama 14)

## SEHEMU D: HADITHI FUPI

**A. Chokocho na D. Kayanda**: *Tumbo Lisiloshiba na Hadhithi Nyingine*

*Jibu swali la 6 au la 7.*

**Said A. Mohamed:** "*Tumbo Lisiloshiba*"

6. "...lakini hakuiruhusu sahau iketi na kutawala kichwani mwake...hapoi...Angepoaje na ule moto unaomlipukia kila mtu pale mtaani, umeacha mpaka sasa kovu bichi moyoni mwa kila mtu...?"

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Bainisha tamathali **tatu** za usemi ambazo zimetumiwa katika kauli hii. (alama 3)

(c) Fafanua sifa **tano** za mhusika anayerejelewa na kauli hii. (alama 5)

(d) Huku ukijadili hoja **nane**, onyesha jinsi wakazi wa Madongoporomoka walivyolipukiwa na moto. (alama 8)

**7.** Onyesha jinsi maudhui ya utabaka yalivyoshughulikiwa katika *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine* kwa kurejelea hadithi zifuatazo:

(a) Mkubwa (alama 12)

(b) Kidege (alama 8)

## SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

**8.** (a) *Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.*

Nalilitizama jua la kinjano
Likijikokota kwa jitimai kutua
Mbele ya nguu
ya mlima uso kikomo
likipisha machweo
yenye giza la kaniki
Likishindilia uzito wa nanga
kwenye moyo tepetevu
uloonja shubiri ya kwondokewa.

Twalitazamana na hiyo shamsi
ikipotelea kwenye upeo wa macho
huku nyuma ikinambia
"yamekwisha.".
Naliona kope zake zikimezwa na kiza
Nikaliona jua likitoweka pamwe nawe
Jagina wa maisha yangu.
Nikaliona likikokota aushiyo
likabwakura rohoyo
kutoka kwenye vyangu vitanga.

Kumbukizi zilikuleta
kwenye jukwaa la akili yangu
pazia likafunguka
likayaleta mawio
ya siku ya kuamkia kuuka kwako.
Nalikuona kwenye ruya ukitazamana ana kwa ana
na hasidi alokakawana
kutuhasiri mi nawe
Nalikiona kipaji chako
kikitwaa wasiwasi
ukawa ni kama wanywea
kwa wake mtazamo.

Hata uliponishika
mkono kunambia
tukimbile tujiponye
nalikuwa nimechelewa
ulikuwa keshanipa kisogo, huku
nyuma waniita,
"Mwanangu, njoo tujisalimishe
Mwanangu njoo, nguvu zimenisha."
Kumbe hiyo ilikuwa tahadhari
kwamba Iziraili yu karibu
moyowe kuchukua?
Kumbe wali ukisema,'Buriani mwanangu?"

Siku ya faradhi ilifika, mkono kulazimika kukupungia
Naliutazama mwilio mtukufu
Nalilitazama tambolo liloumbuka
wali umedhibitiwa shujaa wangu
ndani ya chumba chenye kuta
na paa la mbao.
Hata tulipokukaribisha,
kwa lako kaburi
Nilijipa kujiambia, "Hajenda popote
mtima bado wapiga."
Nalingoja unisalimu
Nalingojea tabasamu lako lenye haya
Ela hayo hayakutimila
Walikuwa kesha kwenda
Kuwa milki, ya ardhi isoshiba.

Hata waliponena, "Udongo kwa udongo,"
Nilikusikia ewe yeli uso kifani
ukighani ubeti wa wimbo
wako pendwa mawazoni mwangu,
"Kifo ni hasidi,
Ikiwa mimi Gunge
Roho yangu nitamkabidhi Iziraili
Mimi niliyekaidi bunduki ya Mzungu
Katika kitali cha miaka minne
Kwetu kukarudi fahari na jina.
Mimi niliyeshindana na ndui na tetekuwanga, iliyowapukutisha
wana wote wa Ngome
Nikabaki mimi, jogoo wa kijiji.

"Kifo ni shujaa,
Ikiwa mimi Gunge mwili wangu huu mtukufu
kwa tambo na nemsi
nitaukubalia
kuwa lengo la dua za kuonewa imani
kuwa karamu ya macho ya mahasimu
kuvikwa suti na mwosha
kufunikwa kwa udongo uliolaaniwa
Mimi Gunge,
Niliruhusu jabali kubwa
Likibinye changu kichwa
Likidhibiti changu kidari
Linizibe zangu pumzi
Gunge niache kutawala."

(i) Huu ni wimbo wa aina gani? (alama 1)

(ii) Andika sababu **mbili** kuthibitisha jibu lako la a(i). (alama 1)

(iii) Ni nani anayeimbiwa na nafsineni? (alama 1)

(iv) Bainisha matatizo **mawili** yanayoikumba jamii inayosawiriwa na utungo huu. (alama 2)

(v) Bainisha mbinu zifuatazo katika wimbo huu. (alama 3)

I. ritifaa

II. mbinu rejeshi

III. taashira

(vi) Unanuia kutumia mbinu ya kutazama na kushiriki kufanya utafiti kuhusu nyimbo za aina hii. Eleza sababu **sita** za kuchagua mbinu hii. (alama 6)

(b) Fafanua mikakati **sita** ambayo jamii inaweza kutumia ili kuudumisha utanzu wa semi. (alama 6)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.**